**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**
**Imezuiwa hadi Septemba 19, 2013 saa 5 asubuhi**

# Wananchi wameshazoea kukosekana kwa dawa, wasema wahudumu wa afya na wagonjwa

## Ila wananchi wanajitahidi kutafuta njia mbadala za kujipatia dawa wanazohitaji

**Septemba 19, 2013, Dar es Salaam:** Karibu wagonjwa wote (97%) wanaofika katika vituo vya afya huandikiwa dawa, au maelekezo ya dawa ama kupewa vyote kwa pamoja. Hata hivyo, wagonjwa wawili kati ya watano (41%) wanaripoti kutokufanikiwa kupata dawa walizoandikiwa. Kukosekana kwa dawa kunatajwa kuwa ni moja kati ya matatizo makuu kwenye utoaji huduma bora, ikiwa asilimia 69 ya wahudumu wa vituo vya afya wakilitaja kuwa ndilo tatizo kuu kwao. Wakati huo huo, karibu wagonjwa wote (99%) waliripoti kuwa mwishoni waliweza kuzipata dawa walizozihitaji mahali tofauti na vituo vya afya. Pengine hii ina maana kuwa wananchi huenda kwenye maduka ya dawa binafsi ili kuziba pengo la kukosekana kwa dawa katika vituo vya afya vya umma.

Matokeo haya yalitolewa na shirika huru la Twaweza katika muhtasari wa utafiti uitwao *Dawa zipo au zimeisha? Upatikanaji wa dawa Tanzania*. Muhtasari huu ulijikita kwenye takwimu kutoka kwenye utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti kwa njia ya simu za mkononi uliowakilisha Tanzania Bara.

Upatikanaji wa dawa ulionekana kuwa suala lililogusa maisha ya mamilioni ya wananchi kutokana na familia mbili kati ya tatu nchini Tanzania kuripoti kuwa walau mwanakaya mmoja aliugua katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* ulilenga kujua ni wapi wananchi walipata matibabu na kwa namna gani walipata dawa walizozihitaji. Pia ulilenga kubaini kama watumishi wa afya walikuwa na mchango katika kuzuia au kuhamasisha utoaji wa dawa kwa wagonjwa.

Matokeo yalionekana kutoa habari njema kuhusu chanjo, chanjo zikiwa ni sehemu muhimu katika huduma ya kinga ya afya. Karibu vituo vyote (96%) vya afya viliripoti kutoa chanjo, asilimia 80% ya vituo hivyo vikiwa pia na akiba ya kutosha ya chanjo hizi. Zaidi ya hayo, nusu ya wagonjwa wote waliotembelea vituo vya afya na kukutwa na malaria, waligundua kuwa idadi kubwa (90%) ya vituo hivi vilikuwa na akiba nzuri ya dawa ya kutibu malaria (Alu).

Lakini siyo taarifa zote zilizotoa matokeo mema. Utafiti wa viashiria vya Utoaji Huduma ya mwaka 2010 ulionyesha kuwa robo (24%) ya dawa muhimu, kwa wastani, hazikuwepo kwenye vituo vya afya nchini kote. Vivyo hivyo, dawa aina ya Alu, ambayo ilitolewa kwa punguzo kupitia mpango wa Serikali na wahisani, mara nyingi ilikuwa ikiuzwa kwa bei ya juu zaidi kuliko hiyo iliyokuwa imeteuliwa. Ni vituo vya afya asilimia 37 tu, na maduka ya dawa asilimia 29 tu yaliyokutwa yakiuza dawa hii kwa bei iliyopendekezwa na serikali.

Wakuu wa vituo vya afya walisema utoaji huduma bora za afya kwa kiasi kikubwa kulikuwa kunakwamishwa na kukosekana kwa dawa, hata hivyo hakukuwa pia na ufuatiliaji mzuri wa dawa

zilizokosekana. Asilimia 52% tu yao ndiyo waliopeleka taarifa za kukosekana kwa dawa kwenye Baraza la Menejimenti ya Afya na 7% walioripoti kutofanya chochote pale akiba ya dawa ilipoisha.
Jambo lililotia shaka ni kuwa zaidi ya robo ya wagonjwa (28%) waliripoti kuwa walinunua dawa katika maduka ya dawa ambayo yalimilikiwa na watumishi wa vituo cha afya au ndugu waliohusiana na watumishi wa vituo vya afya. Ingawa hakukuwa na sheria zilizowazuia wanafamilia wa watumishi wa vituo vya afya kumiliki maduka ya dawa, bado hili linaweza kuleta mgongano wa kimaslahi.

*"Inatia moyo kuona dawa za kutibu malaria na chanjo zikipatikana kwa wingi."* Alisema Elvis Mushi, mtafiti wa Twaweza "*Hata hivyo, kukosekana dawa zingine, na vikwazo vya kupata dawa vilivyotajwa na wagonjwa na wafanyakazi wa vituo vya afya ni changamoto muhimu zinazopaswa kushughulikiwa katika mfumo wetu wa utoaji huduma za afya."*

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema: "*Takwimu zetu zinaonyesha kuwa hata pale huduma za afya zilipokuwa zinakwama, wananchi walijitahidi kutafuta njia mbadala za kukabiliana na mapungufu hayo ili wapate dawa na huduma. Lakini mwananchi hawezi kuwa na uhakika wa ubora na vipimo au kujua madhara ya huduma zinazotolewa nje ya vituo vya afya. Serikali haina budi kutafuta njia ya kutatua tatizo hili."*

Muhtasari wa Twaweza unaeleza pia matokeo mengine mbalimbali ya utafiti huu ambayo yanaweza kupakuliwa hapa www.twaweza.org/sauti

**---- Mwisho ----**

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na :**
Risha Chande
Meneja Mawasiliano, Twaweza
**baruapepe:** rchande@twaweza.org | **simu:** (+255) (0) 656 657559

**Maelezo kwa Wahariri**

Muhtasari huu na data vinapatikana pia kupitia www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayoamsha msukumo wa kiraia na ambayo inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika ya Mashariki. Twaweza inaamini kwamba mabadiliko ya kudumu huhitaji msukumo unaoanzia chini, na inatafuta kukuza hali na kupanua fursa ambazo kwazo mamilioni ya watu wanaweza kupata taarifa na kufanya mabadiliko hayo yatokee katika jamii zao na hasa kwa kuziwajibisha serikali moja kwa moja.
Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
**Tovuti:** www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi